

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Simu Na: +255 (026) 2963630  
Nukushi: +255 (026) 2963629  
Barua Pepe : ps@utumishi.go.tz



Menejimenti ya Utumishi wa Umma na  
Utawala Bora  
Jengo la Taaluma Na.1,  
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria,  
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),  
Barabara ya Mkalama,  
S.L.P. 670,  
**40404 DODOMA**

Tovuti : <http://www.utumishi.go.tz>

*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb. Na. TG 472/535/01/A/66

16 Agosti, 2017

Makatibu Wakuu Wote,  
Makatibu Tawala wa Mikoa Wote,  
Wakuu wa Idara za Serikali Zinazojitegemea Wote,  
Wakuu wa Wakla za Serikali Zote,  
Wakurugenzi wa Halmashauri za Majiji, Manispaa,  
Wilaya na Miji Wote,  
Wakuu wa Taasisi Zote za Umma,  
**TANZANIA BARA.**

**YAH: KUWATAMBUA WATAALAM WA TEHAMA WALIOPO  
KATIKA TAASISI ZA UMMA**

Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kisera, kisheria, kimkakati na kiutendaji katika kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kurahisisha utendaji wake na kuboresha utoaji wa huduma zake kwa wananchi. Kasi kubwa ya maendeleo na mabadiliko katika nyanja hiyo, imeleta ongezeko la mahitaji ya mbinu mpya za utendaji zenye tija na ufanisi katika Taasisi za Serikali. Hali hii inaleta umuhimu wa kuwa na wataalamu waliobobea na wenye misingi ya weledi katika fani ya TEHAMA ambao wataendana na kasi ya maendeleo hayo na pia kukidhi haja na majukumu katika sekta mbalimbali.


2. Katika jitihada za kuwa na wataalamu waliobobea na wenye misingi ya weledi na kuweka mifumo ya usimamizi na uendelezaji wa stadi kwa

wataalamu wa TEHAMA katika Taasisi za Umma, Serikali inakusudia kufanya utambuzi wa wataalamu wote wa TEHAMA ili kubaini uwezo wao pamoja na namna wanavyoendana na Miundo ya Maendeleo ya Kada ya TEHAMA iliyopo katika Taasisi za Umma. Hatua hii itaiwezesha Serikali kubaini vipaji, kuweza kuwasimamia vema, kuwajengea weledi na uwezo na pia kuendeleza stadi za wataalamu wa TEHAMA katika Taasisi za Umma.

3. Zoezi hili la utambuzi litahusisha wataalam hao kutakiwa kujaza taarifa zao kwenye mfumo wa wataalam wa TEHAMA Serikalini unaopatikana kupitia anuani ifuatayo: [ictexpert.gov.go.tz](http://ictexpert.gov.go.tz).

4. Hivyo kwa barua hii, naelekeza uwahimize wataalam wote wanahohusika na kazi za TEHAMA katika Taasisi yako wajaze taarifa zao katika mfumo huo kabla au ifikapo tarehe 15 September, 2017.

Ninawashukuru kwa ushirikiano wenu.



Dkt. Laurean Ndumbaro  
**KATIBU MKUU (UTUMISHI)**

Nakala: Katibu Mkuu Kiongozi,  
Ofisi ya Rais.  
IKULU,  
1Barabara ya Barack Obama,  
S.L.P. 9120,  
**11400 DAR ES SALAAM.**